

Je, mtoto wako mvulana au msichana ni wa kwanza katika familia yako kwenda katika chuo nchini Marekani? Tunatambua kwamba ingawa hii inaweza kuwa hatua ya kufurahisha, na sisi, katika Simpson College, tunataka wewe na familia yako mjiandae na kufanya uamuzi bora kuhusu mahali pa kwenda kupata elimu ya juu na mambo ambayo familia yako inaweza kutarajia.

Simpson College inatoa mipango na huduma nyingi za kusaidia wanafunzi wote kufaulu katika elimu yao.

1. **Kituo cha Nyenzo za Elimu (Center for Academic Resources)** – kuanzia kwa mafunzo ya bure hadi kwa mwongozo wa kufanya utafiti, tuko pamoja katika kila hatua ya safari yako ya mafanikio

Tunatoa huduma za usaidizi wa elimu kwa wanafunzi wote wa Simpson College. Masomo yote makuu. Masomo yote ya GPA. Uwezo na viwango vyote vya elimu. Iwe unatafuta huduma za ufikivu/walemaavu, usaidizi wa kusomea mitihani, mafunzo ya somo maalum, ushauri wa elimu au mwongozo wa kufanya utafiti, timu yetu iko tayari kusaidia.

2. **Somea Nje ya Nchi (Study Abroad)** – mafunzo ya utamaduni na lugha maarufu ulimwengu

Waajiri wa sasa wanatafuta watu walio na maarifa ya kimataifa na uzoefu wa moja kwa moja wa tamaduni zingine. Hii ndio sababu Simpson inathamini zaidi hali za wanafunzi wetu za kusomea nje ya nchi. Kwa kusomea nje ya nchi, unaweza kupanua ufahamu wako wa ulimwengu, kujifunza kukubali tamaduni zingine tofauti na wako, kuwa na mtazamo mpya kuhusu utamaduni wako, kukuza ustadi wako wa lugha nyingine na kupata hisia mpya ya kujamini.

Mipango yote ya kusomea nje ya nchi inaongozwa na maprofesa wa Simpson na ni wazi kwa wanafunzi wote wa Simpson bila kujali wanachosomea.

3. **Huduma za Afya na Ushauri** – Bidhaa na huduma za bure na za bei nafuu zinapatikana kwa wanafunzi. Hii ni pamoja na, lakini si tu, huduma za kwanza za dharura, uchunguzi wa ugonjwa na jeraha, vifaa na nyenzo za elimu ya afya. Ofisi ya Huduma za Ushauri ya Chuo cha Simpson (Simpson College's Office of Counseling Services) inapatikana kwa wanafunzi kwa huduma za ushauri wa ana kwa ana na kuititia kwa simu au video. Ukipenda, tuko tayari pia kutoa msaada wa uelekezaji kwa huduma katika jamii yako.

4. **Huduma za Usaidizi kwa Wanafunzi (TRIO)** – Kutoa Msaada kwa jamii ambazo hazipati huduma za kutosha

Huduma za Usaidizi kwa Wanafunzi za TRIO (TRIO Student Support Services) ni mpango unaofadhiliwa na serikali ya shirikisho uliobuniwa ili kutoa msaada wa elimu, shughuli za utamaduni na mpango wa ukuaji wa binafsi kwa jamii ambazo kimsingi hazipati huduma za kutosha ambazo mara nyingi hukabiliwa na vizuizi vya kupata elimu ya juu: wanafunzi wa wazazi ambao hawakumaliza chuo, kutoka jamii za mapato ya chini na wenye uwezo tofauti. Kuna orodha ndefu ya faida za mpango huu. Huduma ni za bure kwa wanafunzi, lakini lazima watume maombi.

5. **Msaada wa Fedha na Karo ya Masomo** – Usiwe na wasiwasi. Hatalipa karo yote masomo hapa – hata haitakaribia!

Kila mwanafunzi wa Simpson anastahiki kupata ufadhili wa masomo, kuanzia kiasi cha \$22,000. Huo ni mwanzo tu! Tumeunda AHADI YA SIMPSON (SIMPSON PROMISE) kama ahadi ya kudumisha unaifuu. Inalipia karo yote ya masomo (ikiwa ni pamoja na msaada wa ruzuku na ufadhili wa masomo wa Simpson, jimbo na shirikisho) kwa wanafunzi wa Iowa wanaostahiki. Mipango hii ina thamani kubwa mno kwa maisha ya usoni ya mtoto wako. Simpson ni chuo nambari #1 katika jimbo la Iowa kwa mapato ya wanafunzi wa zamani mwaka mmoja baada ya kumaliza chuo.

Kwa nyenzo za ziada, tembelea tovuti hii: Mambo 5 Ambayo Wazazi Ambao Hawakumaliza Chuo Wanapaswa Kujua Kuhusu Chuo

<https://scholarshipamerica.org/blog/5-things-first-generation-parents-should-know-about-college/>